# Ofisi ya Taifa ya Takwimu

S. L. P 796 Simu: 255- (022) 2122722/3/4 Nukushi:+225 (022)2130852
Dar es Salaam,-TANZANIA Barua pepe: dg@nbs.go.tz


***Unapojibu tafadhali taja*:**
**Kumb Na: NBS/S.40/21/462**

**YALIYOJITOKEZA**

**Tarehe: 15 Machi, 2012**

## FAHIRISI ZA BEI ZA TAIFA MWEZI FEBRUARI, 2012

### Utangulizi

### Maana ya Fahirisi za Bei za Taifa

Fahirisi za bei za Taifa ni kipimo kinachotumika kupima mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma mbalimbali zinazotumiwa na jamii. Bei za bidhaa na huduma zipatazo 224 hukusanywa kila mwezi kwa kila mkoa nchini.

### Mizania mpya za bidhaa na huduma za jamii na kizio cha bei

Mizania ya Fahirisi za bei za Taifa zimetokana na matumizi ya kaya binafsi kutoka mikoa 21 ya Tanzania Bara. Mizania inajumuisha matumizi ya kaya zote binafsi kutoka mijini na vijijini. Kizio cha Fahirisi za Bei za Taifa kimebadilishwa kutoka Desemba 2001=100 hadi Septemba 2010=100.

### Makundi ya bidhaa na huduma za jamii

Marejeo ya Fahirisi za Bei za Taifa yamefanyika kwa kufuata makundi yaliyokubalika Kimataifa yanayoitwa mchanganuo wa matumizi binafsi "Classification of Individual Consumption by Purpose (COICOP)". Fahirisi mpya za Bei inajumuisha makundi 12 ya mfumo wa COICOP pamoja na fahirisi za bei kwa makundi maalumu. Makundi hayo maalumu ni; 1) Vyakula na vinywaji baridi—vikijumuisha vyakula vinavyoliwa majumbani na mahotelini; 2) Nishati na Mafuta - kundi hili linajumuisha umeme na aina nyingine za nishati zinazotumika majumbani pamoja na petroli na dizeli; 3) Fahirisi za bidhaa na huduma zote za jamii isipokuwa vyakula na vinywaji baridi; 4) Fahirisi za huduma zote za jamii isipokuwa vyakula, vinywaji baridi, nishati na mafuta.

### Namna ya kukokotoa Fahirisi za Bei za Taifa

Maboresho yamefanyika kwenye ukokotoaji wa Fahirisi mpya za Bei za Taifa, ikiwa ni pamoja na kutumia wastani wa jiometria "geometric means" kwenye kukokotoa Fahirisi za Bei katika ngazi za mwanzo badala ya wastani wa kawaida "arithmetic mean", matumizi ya mfumo ulioboreshwa wa ukokotoaji pamoja na mfumo mzima wa kukusanya na kuchambua bei. Kanuni ya "modified Laspeyres index" inaendelea kutumika kukokotoa Fahirisi za Bei za Taifa katika ngazi ya makundi makubwa.

## MFUMUKO WA BEI KWA KIPIMO CHA MWAKA UMEPUNGUA KIDOGO HADI ASILIMIA 19.4

### Jedwali Namba 1: Badiliko la Fahirisi za Bei za Taifa kwa Mwezi Februari 2012 (Septemba 2010 = 100)

| Na. | KUNDI (MAIN GROUP) | Mizania (Weight) | Feb-2011 | Jan - 2012 | Feb - 2012 | Badiliko la mwezi mmoja | Badiliko la miezi 12 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Vyakula na vinywaji baridi | 47.8 | 109.32 | 135.72 | 138.47 | 2.0 | 26.7 |
| 2 | Vinywaji vyenye kilevi na bidhaa za tumbaku | 3.3 | 102.51 | 107.35 | 111.04 | 3.4 | 8.3 |
| 3 | Mavazi ya nguo na viatu | 6.7 | 103.75 | 115.40 | 118.21 | 2.4 | 13.9 |
| 4 | Nishati, Maji na Makazi | 9.2 | 104.45 | 123.34 | 124.82 | 1.2 | 19.5 |
| 5 | Samani, vifaa vya nyumbani na ukarabati wa nyumba | 6.7 | 110.21 | 117.64 | 119.28 | 1.4 | 8.2 |
| 6 | Gharama za Afya | 0.9 | 101.40 | 103.83 | 103.89 | 0.1 | 2.5 |
| 7 | Usafirishaji | 9.5 | 101.58 | 112.34 | 112.64 | 0.3 | 10.9 |
| 8 | Mawasiliano | 2.1 | 97.32 | 98.06 | 96.55 | -1.5 | -0.8 |
| 9 | Utamaduni na Burudani | 1.3 | 99.33 | 103.16 | 107.94 | 4.6 | 8.7 |
| 10 | Elimu | 1.7 | 105.70 | 107.89 | 110.75 | 2.7 | 4.8 |
| 11 | Hoteli na Migahawa | 6.4 | 105.25 | 116.86 | 121.88 | 4.3 | 15.8 |
| 12 | Bidhaa na huduma nyinginezo | 4.5 | 99.45 | 109.06 | 111.52 | 2.3 | 12.1 |
| | **JUMLA – FAHIRISI BIDHAA ZOTE** | **100.0** | **106.41** | **124.64** | **127.05** | **1.9** | **19.4** |
| | **Makundi Mengine Teule** | | | | | | |
| 1 | Vyakula—vikijumuisha vyakula vilivyoliwa majumbani na mahotelini | 51.0 | 108.87 | 133.63 | 136.64 | 2.3 | 25.5 |
| 2 | Nishati na Mafuta—kundi hili linajumuisha umeme na aina nyingine za nishati zinazotumika majumbani pamoja na petroli na dizeli | 5.7 | 100.93 | 132.24 | 134.73 | 1.9 | 33.5 |
| 3 | Fahirisi za bidhaa na huduma zote za jamii isipokuwa vyakula na vinywaji baridi | 49.0 | 103.50 | 114.00 | 115.70 | 1.5 | 11.8 |
| 4 | Fahirisi na huduma zote za jamii Isipokuwa vyakula, nishati na mafuta | 43.3 | 103.89 | 111.26 | 112.84 | 1.4 | 8.6 |

Mfumuko wa Bei wa Taifa wa mwaka unapima kiwango cha badiliko la kasi ya bei za bidhaa na huduma zote zinazotumiwa na kaya binafsi. Jedwali namba 1 hapo juu linaonyesha kwamba, mfumuko wa bei wa Taifa kwa mwezi Februari 2012 umepungua hadi asilimia 19.4 kutoka asilimia 19.7 kwa mwezi Januari 2012. Kupungua kwa Mfumuko wa Bei wa mwezi wa Februari 2012 kunamaanisha kuwa, kasi ya upandaji wa bei za bidhaa na huduma kwa mwezi Februari 2012 imepungua ikilinganishwa na kasi ya kupanda kwa bei kwa mwezi Januari 2012. Hata hivyo, kwa ujumla Fahirisi za bei zimeongezeka hadi 127.05 mwezi wa Februari 2012 kutoka 106.41 mwezi wa Februari 2011. Mfumuko wa bei wa Vyakula na Vinywaji Baridi umepungua hadi asilimia 26.7 mwezi wa Februari 2012 kutoka asilimia 27.8 kwa mwezi wa Januari 2012.

### Mfumuko wa Bei kwa Bidhaa za Vyakula na Bidhaa Zisizo za Vyakula


Badiliko la Fahirisi ya Bei za bidhaa za vyakula majumbani na migahawani limepungua hadi asilimia 25.5 mwezi wa Februari 2012 ikilinganishwa na asilimia 26.2 mwezi wa Januari 2012. Kasi ya ongezeko kwa bidhaa zisizo za vyakula imebakia kuwa asilimia 11.8 kwa mwezi wa Februari 2012 kama ilivyokuwa mwezi wa Januari 2012.

## Mfumuko wa Bei wa Bidhaa na Huduma Zote Isipokuwa Bidhaa za Vyakula na Nishati

Aina hii ya Fahirisi haijumuishi vyakula vilivyoliwa majumbani na migahawani, vinywaji baridi, petroli, dizeli, gesi ya kupikia, mafuta ya taa, mkaa na umeme. Vyakula na nishati vina sifa ya kuwa na bei ambazo hubadilika mara kwa mara hivyo vikiondolewa kwenye Fahirisi ya bidhaa na huduma zote hubakia Fahirisi ambayo ina mwelekeo imara kwa watunga sera.

Mfumuko wa bei ambao haujumuishi vyakula na nishati kwa mwezi wa Februari 2012 umepungua hadi asilimia 8.6 kutoka asilimia 9.0 kwa mwezi wa Januari 2012. Kwa upande mwingine, mfumuko wa bei wa nishati umeongezeka hadi asilimia 33.5 kwa mwezi wa Februari 2012 kutoka asilimia 30.1 kwa mwezi wa Januari 2012. Kuongezeka kwa mfumuko wa bei wa nishati kumesababishwa hasa na kuongezeka kwa bei za umeme kwa asilimia 36.7.

**Kielelezo Namba 1: MWELEKEO WA FAHIRISI ZA BEI ZA TAIFA NA MFUMUKO WA BEI KUTOKA FEBRUARI, 2011 HADI FEBRUARI, 2012. (SEPTEMBA 2010 = 100)**




Kielelezo namba 1 hapo juu kinaonesha kuwa, katika kipindi kati ya Februari 2011 hadi Februari 2012, kumekuwa na mwenendo wa kuongezeka kwa bei za bidhaa na huduma mbalimbali kama inavyoonyeshwa na Fahirisi za bei. Mfumuko wa bei umekuwa na mwenendo wa kupanda kutoka asilimia 7.5 mwezi Februari 2011 hadi kufikia asilimia 19.7 mwezi Januari 2012 na kupungua kidogo hadi asilimia 19.4 mwezi Februari 2012.

## MFUMUKO WA BEI KWA KIPIMO CHA MWEZI UMEONGEZEKA KWA ASILIMIA 1.9

Mfumuko wa Bei wa mwezi Februari 2012 umeongezeka kwa asilimia 1.9. Fahirisi za Bei zimeongezeka hadi 127.05 mwezi Februari 2012 kutoka 124.64 mwezi Januari 2012. Kuongezeka kwa mfumuko wa bei kumechangiwa na kuongezeka kwa bei za bidhaa za vyakula na zisizo za vyakula. Baadhi ya bidhaa za vyakula zilizochangia kuongezeka kwa bei ni pamoja na mchele kwa asilimia 6.3, vitafunwa kwa asilimia 5.0, mahindi kwa asilimia 5.0, unga wa mahindi kwa asilimia 4.8, ulezi kwa asilimia 7.0, nyama kwa asilimia 4.0, nyama ya nguruwe kwa asilimia 5.1, mayai kwa asilimia 5.5, mapapai kwa asilimia 5.4, mbogamboga kwa asilimia 3.3, chai migahawani kwa asilia 4.7, maji ya kunywa kwa asilimia 5.9 na juisi ya matunda kwa asilimia 4.7. Kwa upande

mwingine, baadhi ya bidhaa zisizo za vyakula zilizochangia kuongezeka kwa bei ni pamoja na bia kwa asilimia 4.5, mavazi kwa asilimia 2.6, viatu kwa asilimia 1.7, umeme kwa asilimia 36.7, seti ya sofa kwa asilimia 4.0, mashuka kwa asilimia 4.3, jiko la gesi kwa asilimia 3.1, vipuri vya vyombo vya usafiri kwa asilimia 2.6, kamera kwa asilimia 8.0, magazeti kwa asilimia 29.2, vyakula migahawani kwa asilimia 4.3, sabuni za kuogea kwa asilimia 8.6 na gharama za kusaga nafaka kwa asilimia 3.3.


## Thamani ya Shilingi ya Tanzania Mwezi Septemba 2010 Ikilinganishwa na Mwezi Februari 2012

Tafsiri: Thamani ya Shilingi ya Tanzania inapima badiliko la uwezo wa Shilingi ya Tanzania katika kununua bidhaa na huduma mbalimbali za mlaji ambazo Shilingi ya Tanzania itaweza kununua katika vipindi tofauti. Ikiwa wastani wa Bei za Taifa (Fahirisi) unaongezeka, thamani ya fedha hupungua.

Thamani ya shilingi 100 imepungua kutoka mwezi Septemba 2010 hadi kufikia Shilingi 78 na senti 71 mwezi Februari 2012.

## MIENENDO YA BEI

### Kielelezo Namba 2: Mienendo ya Bei kwa Makundi Mbalimbali ya Fahirisi za Bei




Kielelezo namba 2 hapo juu kinaonyesha mienendo ya bei kwa makundi mbalimbali ya fahirisi za bei kuanzia mwezi Februari 2011 hadi mwezi Februari 2012. Kwa wastani, Fahirisi za vyakula na vinywaji baridi na Fahirisi za nishati na mafuta zimekuwa na mwenendo wa juu kwa kipindi chote zikilinganisha na fahirisi zingine. Kundi la nishati na mafuta limeonyesha pia kuwa na mwenendo wa fahirisi usio imara ikilinganishwa na makundi mengine kwa kipindi husika. Fahirisi za bidhaa zisizo za chakula na fahirisi za bidhaa zisizo za chakula pamoja na nishati zimeonesha mwenendo wa bei ulio imara.

**Mawasiliano: Mkurugenzi Mkuu,**

**Ofisi ya Taifa ya Takwimu**